

MAKAO MAKUU

Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

TANGAZO KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA MJI WA SINGIDA ("Singida WSSA") KWA MWAKA 2018/19 – 2020/21

Maombi ya mabadiliko ya Bei Na. TR-W-18-001

Mnamo tarehe 29 Machi 2018, Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea ombi kutoka kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Mji wa Singida (Singida WSSA) la kutaka kuongeza bei ya huduma zake za majisafi kwa mwaka 2018/19 hadi 2020/21. Jedwali namba 1 hadi 5 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na zinazopendekezwa.

Jedwali 1: Bei za za Maji sasa na zinazopendekezwa (shilingi kwa mita moja ya ujazo)

Aina za Wateja	Matumizi (M3)	Bei za Sasa	Bei zilizopendekezwa					
		2017/18	2018/19	2019/20	2020/21	Badiliko		
							badiliko	Badiliko
Majumbani	0-10	1,040	54%	1,600	0%	1,606	1%	1,620
	>-10	1,220	39%	1,700	1%	1,710	0%	1,715
Biashara	0-10	1,220	39%	1,690	1%	1,710	1%	1,730
	>-10	1,315	37%	1,800	1%	1,810	1%	1,820
Taasisi	>-10	1,395	29%	1,800	1%	1,810	0%	1,815
Taasisi za Kidini	0-10	1,220	38%	1,680	0%	1,685	0%	1,690
	>-10	1,315	34%	1,760	0%	1,760	1%	1,780
Magati	-	2,125	6%	2,250	0%	2,250	0%	2,250
Viwandani		2,125	41%	3,000	0%	3,000	0%	3,000
Kioski		1,065	182%	3,000	0%	3,000	0%	3,000
Ujenzi		2,125	41%	3,000	0%	3,000	0%	3,000

Jedwali 2: Gharama ya Huduma ya Sasa na Iliyopendekezwa (shilingi/mwezi)

Aina za Wateja	Bei za sasa	Bei Zilizopendekezwa					
	2017/18	Badiliko	2018/19	Badiliko	2019/20	Badiliko	2020/21
Majumbani	2,500	-100%	0	0%	0	0%	0
Biashara	3,000	-100%	0	0%	0	0%	0
Taasisi	3,000	-100%	0	0%	0	0%	0
Taasisi za Kidini	3,000	-100%	0	0%	0	0%	0
Viwandani	4,500	-100%	0	0%	0	0%	0
Ujenzi	4,500	-100%	0	0%	0	0%	0

Jedwali 3: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Maunganisho Mapya (Shilingi kwa maunganisho mapya)

Aina za Wateja	Bei za sasa	Badiliko	Tozo zilizopendekezwa kwa miaka mitatu				
	2017/18		2018/19	Badiliko	2019/20	Badiliko	2020/21
Majumbani	Asilimia 20 ya gharama za Vifaa	0%	Asilimia 20 ya gharama za Vifaa	0%	Asilimia 20 ya gharama za vifaa	0%	Asilimia 20 ya gharama za Vifaa
Biashara							
Taasisi							
Viwandani							

Jedwali 4: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Kuhamisha Maunganisho (TZS/Mwezi)

Aina za Wateja	Tozo za Sasa	Badiliko	Tozo zinazopendekezwa				
	2017/18		2018/19	Badiliko	2019/20	Badiliko	2020/21
Wateja wote	20,000	0%	20,000	0%	20,000	0%	20,000

Jedwali 5: Tozo za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kusitishwa (Shilingi kwa marejesho)

Aina za Wateja	Bei za sasa	Tozo Zinazopendekezwa					
	2017/18	Badiliko	2018/19	Badiliko	2019/20	Badiliko	2020/21
Majumbani	20,000	0%	20,000	0%	20,000	0%	20,000
Biashara	40,000	0%	40,000	0%	40,000	0%	40,000
Taasisi	40,000	0%	40,000	0%	40,000	0%	40,000
Ujenzi	40,000	0%	40,000	0%	40,000	0%	40,000
Taasisi za Dini	40,000	0%	40,000	0%	40,000	0%	40,000
Viwandani	40,000	0%	40,000	0%	40,000	0%	40,000

Kutokana na wasilisho la Singida WSSA, bei zinazopendekezwa zitaiwezesha Mamlaka kuongeza mapato ili kumudu gharama za uendeshaji na matengenezo, kupanua mtandao wa usambazaji majisafi kwenye makazi mapya na kuweza kupata fedha za kulipia uchakavu wa miundombinu ya majisafi.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Alhamisi, tarehe 28 Juni, 2018, katika Ukumbi wa Mlade, FDC, Singida Mjini** kuanzia saa **4:00 asubuhi** kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la watumia Huduma zinazodhibitiwa na EWURA na wananchi wote kwa ujumla, kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyooneshwa hapo juu ndani ya kipindi kabla ya tarehe **6 Julai, 2018**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana Makao Makuu ya EWURA, **GHOROFA YA NNE, JENGO LA LAPF, BARABARA YA MAKOLE, DODOMA** au ofisi za Singida WSSA zilizo mjini Singida.

Imetolewa na:
Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)
7 Juni 2018